

# FORM 3 ENDTERM 3 EXAM

## KISWAHILI

### PAPER 3

NAME .....ADM.....CLASS.....

#### MAAGIZO:

Jibu maswali yote kwenye nakala ulizopewa.

#### Ushairi

##### 1. SHAIRI 'A'

Umekata mti mtima  
Umeangukia nyumba yako  
Umeziba mto hasira  
Nyumba yako sasa mafurikoni  
Na utahama  
Watoto Wakukimbia

Mbuzi kumkaribia chui  
Alijigeuza Panya  
Akalia kulikuwa na pala  
Kichwani  
Mchawi kutaka sana kutisha  
Alijigeuza Simba  
Akalia na risasi kichwani

Jongoo kutaka sana kukimbia  
Aliomba miguu elfu  
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa yatakwenda  
Bwanako kumpa sumu ?  
Hadija umeshika nyoka kwa mkia  
Hadija umepitia nyuma ya punda

##### SHAIRI 'B'

Piteni jamani, Piteni haraka  
Nendeni, nendeni huko mwendako  
Mimi haraka, haraka sina  
Mzigo wangu, mzigo mzito mno  
Na chini sitaki kuweka

Vijana kwa nini hampiti ?  
Kwa nini mwanicheka kisogo ?  
Mzigo niliobeba haupo.

Lakini umenipinda ngongo na  
Nendako  
Haya piteni ! Piteni haraka ! Heei !

Mwafikiri mwaniacha nyuma !  
Njia ya maisha ni moja tu.  
Huko mwendako ndiko nilikotoka

Na nilipofikia wengi wenu  
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema  
Niko nyuma ya wakati  
Lakini kama mungepita mbele  
Na uso wangu kutazama  
Ningewambia siti miaka  
Mingi.

- (a) Haya ni mashairi ya aina gani ? Toa sababu
- (b) Washairi hawa wawili wanalamika. Yafafanue malalamishi yao
- (c) Onyesha jinsi kinaya kinavyojoitokeza katika tungo hizi mbili
- (d) Ni vipi Hadija :-
  - (i) Amekata mti mtima ?
  - (ii) Amepita nyuma ya Punda
- (e) Toa mifano 2 ya uhuru wa mashairi kwa kurejelea mashairi haya
- (f) Kwa kurejelea shairi ‘B’ eleza maana ya:-
  - (i) Mzigo
  - (ii) Siri
  - (iii) Kula nimekula
  - (iv) Niko nyuma ya wakati

(al.2)

## 2. *Soma hadithi hii halafu ujibu maswali .*

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme “wanadamu hamtakufa.” Kinyonga alienda kwa mwendo wa kuduwa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akaseme, “Mwanadamu sharti kufa.” Mjusi aliunyanya mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, “Wanadamu sharti kufa!” Akarejelea haraka kwa Mungu. Baada ya muda kinyonga naye akafika duniana na kutangaza, “Wanadamu hamtakufa!” Wanadamu wakapinga mara na kusema, “La! Tumeshapata ujumbe wa Mjusi, wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la mjusi, wanadamu hufa.

### **Maswali**

- (a) (i) Hadithi hii huitwaje?
- (ii) Toa sababu zako

- (b) Eleza **sifa tatu** zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii
- (c) Kinyonga ni mhusika wa aina gani?
- (d) Hadithi hii ina umuhimu gani?
- (e) Taja njia zozote **nne** za kukusanya kazi za fasihi simulizi
- (f) **Tambulisha vipera hivi:-**
  - (i) Kula hepi
  - (ii) Sema yako ni ya kuazima
  - (iii) Baba wa Taifa

3. “**Nilijua ni utoto tu**”

- (a) Fafanua muktadha wa dondo hili (alama 4)
  - (b) Eleza sifa na umuhimu wa mnenaji (alama 20)
4. Onyesha jinsi uongozi mbaya unavyojitokeza katika tamthilia ya Kigogo. (alama 20)